**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

**DKT. SAADA M. SALUM (MBM)**

**AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI MWAKA 2023 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2023/2024**

**JUNI, 2023**

## YALIYOMO

**YALIYOMO ........................................................ i**

**UTANGULIZI ........................................................ 1**

**MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA 2022/2023 ........................................................ 5**

Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2022 ........................ 5
Mwenendo wa Uchumi wa Dunia ........................................ 5
Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Duniani ............................ 7
Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar .................................. 8

**UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 ............. 14**

**MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023 NA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2023/2024 ........................................................ 20**

Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia ........................................ 20
Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar .................................. 20

**MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024 ........................................................ 23**

Maeneo ya Kimkakati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ........ 24

**RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024 ................. 27**

**MAENEO MTAMBUKA ........................................................ 28**

Matumizi ya Matokea ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ........................................................ 28
Uhifadhi wa Mazingira ........................................................ 29
Makundi yenye Mahitaji Maalum (Ulemavu, Dawa za Kulevya na UKIMWI) ........................................................ 29
Tafiti na Ubunifu ........................................................ 31

Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi........................................31
**UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI.........................................................32**
**MAJUMUISHO.........................................................34**
**HITIMISHO.........................................................35**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya dhati, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2022 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2022 hadi Machi 2023) kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024. Pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2022 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Mwaka 2022/2023 kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024.

2. **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii imezingatia Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (Zanzibar Development Plan (ZADEP) 2021-2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025; Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Baraza la Kumi (10) la Wawakilishi na ahadi anazozitoa anapokutana na wananchi; Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) ya Mwaka 2015-2030; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya Mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; pamoja na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063 (African Development Agenda 2063). Kadhalika, hotuba hii inayoelezea Mpango wa Maendeleo wa Taifa ndiyo msingi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 ambayo Serikali itaiwasilisha baadae leo katika Baraza hili Tukufu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa moyo wa dhati, napenda kutoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, uongozi wake wenye dhamira ya dhati ya kuendeleza hali ya amani na utulivu iliopo nchini pamoja na kuinua uchumi wa Zanzibar. Hakika mafanikio ya juhudi zake yanaonekana katika kila sehemu ya Zanzibar. Kwa sasa tunashuhudia namna anavyoendelea kuiongoza Zanzibar kwa amani, mshikamano, busara, hekima na umahiri mkubwa na kuendeleza mashirikiano na nchi mbali mbali. Aidha, niungane na Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani na wananchi wenzangu kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ujasiri na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi wake kikamilifu. Jitihada na uono wake wa kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii katika kuinua hali za wananchi zinaonekana wazi katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.

4. **Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba nitoe shukrani zangu za dhati na kuwapongeza Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla wakiwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais kwa uongozi wao mahiri, usimamizi, uchapakazi na uzalendo kwa nchi yetu. Juhudi zao zinaendelea kuleta mafanikio katika sekta zote nchini. Aidha, nichukuwe fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kusimamia vyema Utumishi wa Umma na kuongoza Kamati ya Makatibu Wakuu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima ya dhati kabisa, naomba nimpongeze Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja

na wasaidizi wake wakuu Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt Philip Isdor Mpango na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kulitumikia Taifa letu. Juhudi za viongozi hawa katika kuiletea Tanzania Maendeleo zinaonekana wazi wazi katika kuisimamia, kuitangaza, kutafuta fedha kupitia kwa Washirika wa Maendeleo na kushajihisha uzalishaji wa ndani kwa kuvutia wawekezaji. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape afya na wepesi viongozi wetu hawa katika kusimamia na kuendelea kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitambue na kushukuru mchango mkubwa wa Baraza lako chini ya uongozi wako Spika Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid ukisaidiwa na Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma pamoja na Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Abdulla Hussein Kombo. Usimamizi wenu unaleta tija katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa maendeleo kwa kufikia malengo tuliyojipangia ambayo yanatokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Abdala Hussein Kombo Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani (CCM) na wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri makini waliotupatia. Maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti yamezingatiwa katika uandaaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2023/2024. Uandaaji wa hotuba hii umepata kwa kiasi kikubwa michango, ushauri na busara za Kamati hiyo. Kwa heshima ya pekee, nawapongeza waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwatumikia vyema wananchi majimboni mwenu. Nasi hatuna budi kulipa fadhila tulizopewa na wananchi kwa kuwaletea maendeleo wanayoyahitaji.

8. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua nafasi hii kutoa mkono wa rambi rambi kwako Mheshimiwa Spika na wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kifo cha Mheshimiwa Habib Mohammed Ali aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe tunamuomba Mungu awape subira ndugu, jamaa na wananchi wa jimbo la Mtambwe kwa kuondokewa.

9. **Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Mwaka 2023/2024 zimezingatia dhana ya ushirikishwaji wa wadau katika hatua za uandaaji na maamuzi katika ngazi zote Serikalini. Ni vigumu kuwataja wadau wote waliotoa maoni na ushauri hadi kufikia hapa lakini mchango na maoni waliyotupatia tumeyazingatia katika uandaaji wa Mpango huu wa Maendeleo.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuhakikisha tunafanikisha Zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi ili kuweza kupata takwimu sahihi ambazo zitatumika katika mipango yetu ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Shukrani za kipekee ziwafikie wadau mbali mbali wa ndani na nje ambao waliwezesha kufanikisha zoezi hili kwa ufanisi zaidi. Nawashauri viongozi wenzangu na wadau wengine kuzitumia takwimu hizi katika mipango yetu ya muda mrefu, wa kati na mfupi ili kuleta maendeleo endelevu.

11. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukrani naomba kuwasilisha kwa muhtasari wa Mapitio ya Hali ya Uchumi ya Mwaka 2022 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2023/2024.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2022 NA UTEKELEZAJIWA MPANGO WA MAENDELEO WA 2022/2023

12. **Mheshimiwa Spika,** Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2022 ni kwa mujibu wa mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla (Macroeconomic Indicators) ikiwemo Pato la Taifa, Kasi ya Mfumuko wa Bei, Hali ya Ajira na Sekta mbali mbali ikilinganishwa na mwaka 2021 na Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 kwa mujibu wa hali ya utekelezaji halisi na kifedha.

### Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2022

### Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

13. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi wa Aprili 2023, kwa mwaka 2022, Uchumi wa dunia umekua kwa kasi ndogo na umefikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.3 mwaka 2021. Hali hii inatokana na mtikisiko wa uchumi kwa nchi zenye uchumi mkubwa duniani kutokana na mgawanyiko uliosababishwa na mgogoro unaoendelea kati ya Urusi na Ukraine; kuongezeka kwa kiwango cha mfumuko wa bei duniani kote; pamoja na kuyumba kwa hali ya kifedha ambayo imezorotesha shughuli za kiuchumi duniani. Vile vile, kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa na kufungwa kwa baadhi ya viwanda kutokana na kupanda kwa gharama za uzalishaji viwandani. Taswira ya ukuaji wa uchumi wa Dunia umegawika katika makundi tofauti kama ifuatavyo:-

   i. Ukuaji wa uchumi kwa Nchi Zilizoendelea umekuwa wa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2021. Hali hii imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa malighafi

ambazo zimesababishwa na kupanda kwa gharama za uzalishaji viwandani.

ii. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi umepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2021. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo, umetokana na kupungua kwa uzalishaji na usafirishaji wa mali ghafi za viwandani pamoja na kupungua kufanya miamala mbali mbali ya manunuzi ya bidhaa na huduma inayohitaji Dola ya Kimarekani;

iii. Kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi za Afrika imepungua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2021. Kasi hiyo ndogo ya ukuaji huu imetokana na kuwepo kwa vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambavyo vimeathiri Uchumi wa nchi nyingi za Afrika. Aidha kushuka kwa thamani ya sarafu za nchi nyingi za Afrika zinazouza bidhaa nje dhidi ya dola za Kimarekani mwaka 2022;

iv. Katika Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, kasi ya ukuaji uchumi kwa mwaka 2022 imekuwa kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 3.9 kutoka wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2021. Hii imetokana na ongezeko la viwango vya juu vya riba vya Kimataifa na kupelekea kuongezeka kwa deni la nje kwa nchi zenye uchumi mkubwa zaidi Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Afrika ya Kusini; na

v. Nchi za Afrika Mashariki, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2021. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kama biashara za nje.

## Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Duniani

14. **Mheshimiwa Spika,** Mfumuko wa bei wa Dunia unaathiri hali ya bei za bidhaa na huduma katika nchi mbali mbali Duniani. Kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta ya Nishati, Madini na huduma kwa mwaka 2022 kumesababisha kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei kufikia wastani wa asilimia 8.7 kutoka wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2021. Hata hivyo, kasi ya mfumuko wa bei una sura tofauti kulingana na maeneo ya kijiografia kama ifuatavyo:

    i. Kasi ya mfumuko wa bei kwa Nchi Zilizoendelea imefikia wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2021. Hii imechangiwa na kupanda kwa bei za nishati kulikopelekea kupungua kwa uzalishaji viwandani;

    ii. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi, kasi ya mfumuko wa bei imepanda na kufikia wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2021. Kupanda kwa mfumuko wa bei kumetokana na kuongezeka kwa bei za chakula na bidhaa za viwandani pamoja na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji wa bidhaa za shambani;

    iii. Kasi ya mfumuko wa bei kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka kufikia wastani wa asilimia 14.5 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 11.0 mwaka 2021. Hii imetokana na kupanda kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, kuongezeka kwa mikopo yenye riba kubwa na nchi hizo kuendelea kuwa na chumi tegemezi; na

    iv. Kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kasi ya mfumuko wa bei imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2021. Kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa muhimu za chakula

na zisizo za chakula kulikosababishwa na uzalishaji mdogo wa ndani, uagiziaji mkubwa wa bidhaa kutoka nje sambamba na kupanda kwa gharama za usafirishaji.

## Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar

15. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Nane chini ya Uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi inaendelea na juhudi kubwa za kuimarisha uchumi kwa maslahi mapana ya Zanzibar na wananchi wake kupitia Sera ya Uchumi wa Buluu. Kwa upande wa Pato Halisi la Taifa (GDP at Constant Prices) kwa mwaka 2022 lilifikia thamani ya TZS 3,498 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 3,275 bilioni mwaka 2021 sawa na kasi ya ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.8 kwa mwaka 2022. Ongezeko hilo ni kubwa ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka 2021. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za soko (GDP at Market price) limeongezeka kufikia thamani ya TZS 5,400 bilioni mwaka 2022 kutoka thamani ya TZS 4,633 bilioni mwaka 2021.

16. **Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa sababu za ukuaji wa Uchumi kwa mwaka 2022 ni pamoja na:

    i. Ukuaji wa sekta ya viwanda kufikia wastani wa asilimia 9.3 kwa mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2021. Ukuaji huu umetokana na ukuaji wa sekta ndogo ya Uchimbaji Mawe na Mchanga (9.1%), Uzalishaji Viwandani (8.1%), Umeme na Gesi (22.3) na Ujenzi (10.2%);

    ii. Kuongezeka kwa Watalii waliotembelea Zanzibar kufikia 548,503 mwaka 2022 kutoka watalii 394,185 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 39;

iii. Kuongezeka kwa thamani ya mazao ya biashara yaliyosafirishwa nje ya nchi. Karafuu zenye thamani ya TZS 118,287.3 milioni mwaka 2022 kutoka TZS 115,358.7 milioni mwaka 2021 zilisafirishwa; na mwani wenye thamani TZS 16,010.2 milioni mwaka 2022 kutoka TZS 11,960.7 milioni mwaka 2021 ulisafirishwa;

iv. Kuongezeka kwa uwekezaji kwa kutekelezwa miradi ya maendeleo yenye thamani TZS 230 bilioni fedha za Mkopo nafuu wa Shirika la Fedha Duniani (IMF). Uwekezaji umefanyika katika miradi ya sekta ya maji, umeme, elimu, afya na uwezeshaji wa wananchi kupitia shughuli za uchumi wa buluu. Vile vile jumla ya TZS 172.1 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimechangia katika ukuaji huu;

v. Kuanza kwa ujenzi wa barabara katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar; na

vi. Kuongezeka kwa maslahi ya watumishi kwa kupandisha mishahara na maslahi yao ambako kumeongeza mzunguko wa fedha na upatikanaji wa mahitaji ya manunuzi mbali mbali katika soko.

17. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makaazi iliyofanyika mwaka 2022, Zanzibar inakadiriwa kufikia idadi ya watu 1,889,773. Wastani wa Pato la Mwananchi limefikia TZS 2.86 milioni sawa na wastani wa USD 1,235 ikilinganishwa na TZS 2.70 milioni sawa na wastani USD 1,171 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 6.0.

## Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar

18. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumuko wa bei kwa mwaka 2022 imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka

wastani wa asilimia 1.7 Mwaka 2021. Kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei kunatokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa zote za chakula na zisizo za chakula. Kwa mwaka 2022 kasi ya bei za bidhaa za chakula zimeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 6.0 kutoka wastani wa asilimia 0.6 mwaka 2021 na kasi ya bei za bidhaa zisizo za chakula zimeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2021.

19. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumuko wa bei ingeweza kuwa ya juu zaidi kama Serikali isingechukua juhudi za kupunguza na kusamehe ushuru kwa baadhi ya bidhaa muhimu ili wananchi waweze kumudu kununua bidhaa hizo muhimu.

20. **Mheshimiwa Spika,** Ruzuku inayotolewa na Serikali kwa bidhaa ya nishati za mafuta imesaidia kupunguza kasi ya mfumuko wa bei na kubakia katika tarakimu moja. Kwa mwaka 2022, Serikali imetoa ruzuku ya TZS 21.5 bilioni kwa bidhaa za mafuta ya nishati na kusamehe ushuru wa mafuta ya kupikia wenye thamani ya TZS 472 milioni pamoja na kupunguza viwango vya ushuru wa sukari kutoka asilimia 25.0 hadi 6.0.

### *Hali ya Ajira*

21. **Mheshimiwa Spika,** Ajira ina mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji wa ndani pamoja na kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Kwa Mwaka 2021/2022, ajira mpya zimefikia 68,632 kutoka ajira 66,656 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 3.0, ambapo ajira kutoka Serikalini zimefikia jumla ya 37,189 ikiwa wanaume ni 15,541 na wanawake ni 21,648 kwa mwaka 2021/2022. Ajira kutoka Mashirika ya Serikali imefikia 6,887 ikiwa wanaume ni 4,522 na wanawake ni 2,365 Mwaka 2021/2022. Kwa upande wa ajira binafsi zimefikia 24,556; wanaume ikiwa ni 15,947 na wanawake ni 8,609 Mwaka

2021/2022. Kuongezeka kwa ajira mpya kumechangiwa zaidi na kuongezeka kwa uhitaji mkubwa wa wafanyakazi kwa Mwaka 2021/2022 katika sekta za elimu, afya na tehama.

***Mwenendo wa Thamani ya Shilingi Dhidi ya Dola ya Marekani***

22. **Mheshimiwa Spika,** thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani imeshuka kwa kasi ndogo sana ukilinganisha na kushuka kwa sarafu nyengine za nchi jirani. Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,303.04 kwa mwaka 2022, sawa na asilimia 0.2 ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,297.93 kwa mwaka 2021. Kushuka huku hakukuwa na athari kubwa sana kwa uchumi wa Tanzania. Vile vile, kulikuwa na ushindani wa kuuza Dola za Kimarekani ambapo wastani Dola za Marekani USD 20 milioni zimeingizwa kwenye Soko la Fedha za Kigeni (Interbank Foreign Exchange Market) kwa ajili ya kusaidia mahitaji ya uingizaji wa bidhaa nchini (import demand) kwa kuzingatia mabadiliko ya thamani ya Fedha kwa kulinganisha na sarafu nyengine ulimwenguni.

***Sekta ya Utalii***

***Uingiaji wa Watalii***

23. **Mheshimiwa Spika,** watalii walioingia nchini katika kipindi cha mwaka 2022 wamefikia watalii 548,503 kutoka watalii 393,512 katika kipindi kama hicho mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 39.4. Ongezeko hili limesababishwa na nchi nyingi kulegeza masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kudhibiti kuenea ugonjwa wa UVIKO 19. Ongezeko la uingiaji wa watalii limechangiwa na ongezeko na mashirika ya ndege kuanzisha safari zao hapa Zanzibar ikichangiwa pia na filamu ya "Tanzania The Royal Tour" ambayo imeitangaza zaidi Tanzania Kimataifa. Kuimarika kwa huduma za viwanja vya ndege pia kumechangia ongezeko la watalii.

vii. **Mheshimiwa Spika,** Nchi ambazo zimeongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2022 ni Ufaransa (watalii 68,487 sawa na wastani wa asilimia 12.48), ikifuatiwa na nchi za Ulaya (watalii 67,917 sawa na asilimia 12.38), Poland (watalii 44,462 sawa na asilimia 8.10), Ujerumani (watalii 43,634 sawa na asilimia 7.95), Italia (watalii 36,928 sawa na asilimia 6.73), Uingereza (watalii 30,552 sawa na asilimia 5.57) na Afrika (watalii 28,583 sawa na asilimia 5.21). Baina ya mwezi wa Julai 2021 hadi Juni 2022, mapato yaliyotokana na utalii yaliyoingia moja kwa moja katika mifumo ya Serikali yalifikia TZS 51.32 bilioni.

***Sekta ya Nje***

**24. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022, nakisi ya biashara imeongezeka hadi kufikia thamani ya TZS 1,078.6 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 812.9 bilioni mwaka 2021, sababu ni kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa kutoka nje kutokana na kuendelea kwa shughuli za uwekezaji ambao umetumia zaidi bidhaa kutoka nje ya nchi. Miongoni mwa bidhaa zilizoagizwa na kuingia nchini ni nishati ya mafuta, vifaa vya ujenzi na bidhaa za chakula. Uagiziaji wa bidhaa zilizoingizwa nchini mwaka 2022, umeongezeka hadi kufikia thamani ya TZS 1,258.9 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 968.6 bilioni mwaka 2021.

**25. Mheshimiwa Spika,** Usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi umeongezeka hadi kufikia thamani ya TZS 180.3 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 155.6 bilioni mwaka 2021, kuongezeka kwa thamani ya usafirishaji ni kutokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu, mwani, viungo (spices) na mazao ya baharini.

### *Mwenendo wa Biashara Baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (Intra trade)*

26. **Mheshimiwa Spika,** Zaidi ya asilimia 50 ya mahitaji ya bidhaa zikiwemo za chakula zinapatikana kutoka Tanzania Bara. Katika kipindi cha mwaka 2022 uhaulishaji wa bidhaa uliimarika na kupelekea upatikanaji wa mahitaji ya bidhaa zote za lazima. Uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 37.6 bilioni kutoka thamani ya TZS 33.9 bilioni mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Kwa upande wa uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 375.8 bilioni mwaka 2022 ikilinganishwa na thamani ya TZS 288.2 bilioni mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 30.3.

### *Ukuzaji Rasilimali*

27. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2022, kumekuwa na ongezeko la miradi ya uwekezaji nchini ambapo Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) iliidhinisha jumla ya miradi 93 yenye thamani ya TZS 4.5 trilioni ikilinganishwa na miradi 97 yenye thamani ya TZS 2.6 trilioni mwaka 2021.

28. **Mheshimiwa Spika**, Kati ya miradi 93 yenye thamani ya TZS 4.5 trilioni iliyoidhinishwa, miradi 35 yenye thamani ya TZS 216.5 bilioni sawa na wastani wa asilimia 38 ya miradi yote inamilikiwa na wazawa na miradi 58 yenye thamani ya TZS 4.3 trilioni sawa na wastani wa asilimia 62 ya miradi yote inamilikiwa na wageni. Miradi hii imechangia katika upatikanaji wa ajira 3,970 mwaka 2022.

29. **Mheshimiwa Spika**, Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa fedha 2022/23 imeongezeka kufikia wanafunzi 1,815 kutoka wanafunzi 1,526 mwaka 2021/22

sawa na ongezeko la asilimia 19. Hii inatokana na kuongezeka kwa wanafunzi ambao wana sifa ya kuendelea na masomo na Serikali kuongeza fungu la mikopo pamoja na ufanisi katika kukusanya marejesho ya wanufaika wa mikopo hiyo.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI MACHI 2023

30. **Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23 ni muendelezo wa Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026. Mpango wenye kaulimbiu inayosema Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu. Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 ulilenga kutekeleza jumla ya Programu na Miradi 86 na kupangiwa jumla ya TZS 1,352.19 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 682.54 bilioni sawa na asilimia 50.47 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka katika vyanzo vya ndani na TZS 669.65 bilioni sawa na asilimia 49.53 zilipangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 62.78 bilioni ni msaada na TZS 606.86 bilioni ni mkopo. Kati ya fedha hizo (TZS 1,352.19) TZS 748.2 bilioni zilipangwa kugharamia Programu na Miradi ya Kimkakati na TZS 603.9 bilioni zilipangwa kutumika kwa Programu na Miradi mengineyo.

31. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha miezi tisa (9) Julai 2022 - Machi 2023, jumla ya TZS 878.9 bilioni sawa na asilimia 65 ya fedha ilipangwa kutumika kwa Programu na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 443.65 bilioni sawa na asilimia 50.5 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani na TZS 435.27 bilioni sawa na asilimia 49.5 zilipangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo. Kati ya TZS 878.9 bilioni, TZS 486.32 bilioni zilipangwa kugharamia

Programu na Miradi ya Kimkakati na TZS 392.52 bilioni zilipangwa kutumika kwa Programu na Miradi mengineyo. TZS 276.04 bilioni sawa na asilimia 31 ya bajeti iliyopangwa ya TZS 878.9 kwa mwaka 2022/23 zilipatikana na kutumika katika kipindi cha Julai 2022-Machi 2023 katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo. TZS 172.1 bilioni sawa na asilimia 39 ya lengo la TZS 443.65 zilipatikana kutoka Serikalini na TZS 12.8 bilioni sawa na asilimia 26 ya lengo la TZS 435.27 bilioni zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

32. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa 2022/23, Serikali ilidhamiria kutekeleza miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi yenye lengo la kuimarisha Ukuzaji wa Uchumi, Miundombinu, Huduma za Jamii na Utawala Bora. Maeneo haya ni yale ambayo yalitarajiwa kuleta matokeo makubwa na kwa haraka ikiwemo upatikanaji ajira nyingi kwa wananchi, kuongeza uwekezaji, kuimarisha hali za wananchi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Kwa kuzingatia maeneo hayo, programu na miradi ya kimkakati kumi na tatu (13) ilipewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023. Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, Programu na Miradi saba (7) ya kimkakati kati ya kumi na tatu (13) iliingiziwa fedha. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya kimkakati kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ni kama ifuatavyo:-

***i. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege - Pemba***

Mradi wa kujenga Uwanja wa Ndege wa Pemba na kuwa Uwanja wa Ndege wenye hadhi ya Kimataifa utakapokamilika. Kufikia mwezi wa Machi, 2023 Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja cha Ndege wa Pemba umeshasainiwa baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya “Propav” kwa kushirikiana na Kampuni ya MECCO. Vile vile, Mkataba wa

Makubaliano ya Mkopo tayari umeshawasilishwa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi ya "United Kingdom Export Finance" (UKEF) kupitia "Citi Bank" kwa ajili ya kuupitia na kusainiwa ili hatua za ujenzi ziweze kuanza.

### *ii. Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu*

Ujenzi wa barabara kuu kwa kiwango cha lami, mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani kwa barabara kuu zenye urefu wa kilomita 125.6 kwa Unguja na Pemba unajumuisha barabara ya Wete – Chake Chake (km 22), Fumba – Kisauni (km 12) na Chake Chake – Mkoani (km 43); na Tunguu - Makunduchi (km 53.). Utekelezaji wa Programu hii imeanza mwaka 2022/23, na imepangiwa jumla ya TZS 249.71 bilioni (TZS 37.95 bilioni kutoka Serikalini na TZS 211.76 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Mkataba wa Ujenzi wa barabara Chake Chake -Mkoani, Tunguu - Makunduchi na Fumba - Kisauni umeshatiwa saini mnamo 19 Septemba 2022. Serikali ya Uingereza chini ya 'United Kingdom Export Finance' (UKEF) imewasilisha Mkataba wa Mkopo (Loan Agreement) kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tayari Serikali imefanya mapitio ya Mkataba huo. Hatua inayoendelea sasa ni Majadiliano ya Mwisho baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mfuko wa Fedha wa Uingereza – UKEF kwa ajili ya kusaini Mkataba wa Mkopo na hatua za ujenzi kuanza. Kwa upande wa ujenzi wa barabara ya Wete - Chake Chake kufikia Machi 2023, jumla ya TZS 11.4 bilioni sawa na asilimia 23 zimepatikana. Kati ya fedha hizo TZS 8.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.4 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (BADEA). Kazi zilizofanyika ni usafishaji wa barabara ya urefu wa kilomita 10.7, kuondosha udongo usiofaa urefu wa kilomita 3, kujenga kitanda cha barabara kwa urefu wa kilomita 3 na ulipaji fidia kwa wananchi 900 kati ya 1,200 waliotathminiwa katika maeneo yatakayoathirika na ujenzi huo.

### *iii. Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani*

Ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo mbali mbali ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Programu imeanza mwaka 2021/22, zinatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitatu (3). Kukamilika kwa barabara hizi kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu; kuunganisha vijiji, mitaa na barabara Kuu; kupendezesha haiba miji na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kurahisisha huduma za usafirishaji wa watu na mizigo pamoja na kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Kwa mwaka 2022/23, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 30.0 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TZS 13.9 bilioni sawa na asilimia 46 zimetolewa kutoka Serikalini. Jumla ya kilomita 18.82 za barabara zimeshakamilika kwa hatua ya kifusi kwa maeneo ya Kidimni-Ubago (km 3.43), Mgenihaji-Kwambani (km 1.87), Mchangani-Dongongwe (km 3.34), Nyamanzi-Cambridge School (km 0.53), Bumbwisudi-Kizimbani (km 2.55), Mwakaje-Mwachealale-Bumbwisudi (km 3.69), Kama Msikitini-Kama KMKM (km 2.29), Upenja-Kibumbwi (km 1.12). Kilomita 2.5 za barabara zinazoendelea na hatua ya kifusi ni Donge Vijibweni-Chaani Masingini (km 2.5). Kilomita 20.96 za barabara zilizokamilika kwa hatua ya lami ni Dimani Sokoni-Dimani Beach (km 1.73), Kombeni-Nyamanzi (km 0.94), Tunguu-Ndijani Mseweni-Mkwajungoma (km 7.49), Jumbi Sokoni-Kibondeni Skuli-Hospitali (km 4.14), Jumbi-IPA-Tunguu (km 4.9), Dunga-Zuze (km 1.76) na Barabara zinazoendelea kwa hatua ya lami ni Cheju-Kibele (km 3.8).

### *iv. Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini*

Matengenezo ya barabara za Mjini yanahusisha uimarishaji wa kilomita 100.9. Programu imeanza mwaka 2022/2023 kwa ujenzi wa barabara za Mkoa wa Mjini Magharibi. Ujenzi utahusisha barabara Kuu, Njia za wapita kwa miguu, Uwekaji wa taa na Ujenzi wa mitaro ya maji. Kukamilika kwa programu hii itakuwa

ni kivutio cha mji, kuimarika kwa sekta ya usafirishaji, biashara na utalii. Kwa Mwaka 2022/2023, programu imepangiwa jumla ya TZS 135.6 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2023, Jumla ya TZS 40.9 bilioni sawa na asilimia 30 zimetolewa kutoka Serikalini. Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini inatekelezwa na Kampuni ya 'China Civil Engineering Construction Corporation' (CCECC) ya China. Ujenzi umeanza kwa barabara ya Chukwani Mwisho – Buyu (km 3.45) na Msumbiji – Kinyang'unya – Mwanakwerekwe (km 5.43) ambazo zipo katika hatua ya usafishaji wa barabara na uwekaji wa fusi tabaka la mwanzo na kuondoa udongo usiofaa. Ujenzi wa barabara ya Uwanja wa Ndege – Mnazi Mmoja umeanza ambayo ni kutoka Mnazi Mmoja hadi Kikwajuni. Kwa upande wa ujenzi wa barabara za juu (Fly Over), hatua inayoendelea kwa sasa ni kufanya vipimo vya udongo (Geotechnical Survey) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo katika maeneo ya mzunguko wa barabara (Round about) za Mwanakwerekwe na Amani.

### *v. Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo*

Mradi huu umeanza mwaka 2021/2022, lengo la mradi ni kuibua na kuendeleza vipaji vya wanamichezo hususan vijana kwa kuweka miundombinu yenye kuhusisha aina mbalimbali za michezo ili kuongeza ushindani wa kimichezo Kitaifa na Kimataifa. Kwa Mwaka 2022/2023, mradi huu umepangiwa TZS 3.0 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2023 kazi zilizofanyika ni kukamilika kwa zabuni pamoja na tathmini kwa ajili ya ujenzi wa viwanja viwili vya michezo (4 in 1) kwa Pemba Wilaya ya Micheweni (Skuli ya Micheweni) na Wilaya ya Chake Chake (Gombani).

### *vi. Uimarishaji wa Huduma za Kijamii*

Katika kuimarisha huduma za kijamii, Serikali kwa kipindi cha Julai – Machi 2023 imetumia TZS 20.8 bilioni. Kati ya fedha hizo,

TZS 15.0 bilioni sawa na asilimia 72.1 kwa ajili ya kukamilisha miradi ya elimu na TZS 1.0 bilioni sawa na asilimia 4.8 kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya afya, miradi ambayo awali ilitekelezwa kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Fedha zilizotolewa na Serikali zilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa uzio na 'landscapping' katika maeneo yaliyojengwa Skuli mpya na Hospitali za Wilaya. TZS 4.8 bilioni sawa na asilimia 23.08 ilitumika kukamilisha ujenzi wa vituo vya wajasiriamali kila Wilaya.

### *vii. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar*

Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar umelenga kusimamia ujenzi wa Ofisi za Serikali katika maeneo yaliyopendekezwa kwa kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi. Programu imeanza mwaka 2019/2020 na TZS 354.4 bilioni kutoka Serikalini zilipangwa kutumika katika programu hii. Kwa mwaka 2022/2023 programu ilipangiwa kiasi cha TZS 92.20, ambazo TZS 75.78 bilioni sawa na asilimia 82.2 kwa ajili ya Ujenzi wa Mji Mpya wa Serikali na TZS 16.42 bilioni sawa na asilimia 17.80 kwa ukamilishaji wa kazi za ujenzi na utanuzi wa Ofisi za Serikali ambazo ujenzi wake ulishaanza. Kwa kipindi cha Julai 2022-Machi, 2023, TZS 817 milioni imetolewa kwa ajili ya malipo ya mwisho katika ujenzi wa Mahakama Kuu - Tunguu. Kwa upande wa ujenzi wa mji wa Serikali utakaojengwa Kisakasaka, taratibu za makabidhiano ya umiliki pamoja na michoro zimekamilika. Kazi za usafishaji wa eneo zimeanza.

33. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa miradi mengine ya maendeleo iliyotekelezwa kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023 unaonekana katika Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi 2022 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2023 NA MPANGO WA MAENDELEO WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2023/2024

### Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

34. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi wa Aprili 2023, kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kukua kwa kasi ndogo kufikia wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Kasi hii ndogo ya uchumi wa dunia itatokana na athari ya vita vinavyoendelea baina ya nchi ya Urusi na Ukraine ambavyo vimeathiri sekta za uzalishaji zikiwemo mafuta na gesi, upungufu wa Dola ya Kimarekani na kuongezeka gharama za usafirishaji wa bidhaa duniani.

### Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar

35. **Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar mwaka 2023 unatarajiwa kuimarika ili kwenda sambaba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatarajia kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na kuimarisha maisha ya wananchi wa Zanzibar, kupitia sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii ikiwemo huduma za elimu, miundombinu, afya na ustawi wa jamii, huduma, kilimo, uvuvi, utalii, biashara na viwanda.

### Malengo na Shabaha za Uchumi Jumuishi kwa Mwaka 2023

36. **Mheshimiwa Spika**, Shabaha za Uchumi Jumuishi zilizozingatiwa katika Mpango  wa mwaka 2023, ni kama ifuatavyo:-

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2023;

ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kubakia katika tarakimu moja;

iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 26.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 24.7 ya mwaka 2022;

iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 22.0 ya Pato la Taifa mwaka 2023 kutoka asilimia 18.1 mwaka 2022; na

v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**37. Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2022 ukuaji huo utatokana na sababu zifuatazo:-

i Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 30 kutoka watalii 548,503 kwa mwaka 2022 hadi watalii 713,053 mwaka 2023;

ii Kuendelea kutekelezwa kwa miradi ya kimkakati ya maendeleo ikiwemo miundombinu ya barabara za mjini na vijijini km 782.9, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, Ujenzi wa bandari ya Mangapwani ambapo kwa sasa wananchi walioathirika na upelekaji wa miundombinu kwa ajili ya ujenzi huo wameanza kulipwa fidia na ukarabati wa bandari ya Malindi ambao utafanywa kwa mashirikiano na sekta binafsi. Miradi mengine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kubakia kwa tarakimu moja;

iv Kuongezeka kwa usimamizi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na matumizi ya Serikali;

v Kuongezeka kwa hatua za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi binafsi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje; na

vi Kuongeza uzalishaji wa ndani kupitia sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya uchumi wa buluu na kilimo.

38. **Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya ukuaji huo unategemea na misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuimarika kwa Sera za kifedha ambazo zitahakikisha upatikanaji wake kwa ajili ya matumizi ya uwekezaji;

ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi katika soko ili kuweza kupunguza gharama za bei;

iii. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama katika nchi jirani; na

iv. Kuendelea kuimarika miundombinu na kuongeza ufanisi katika bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa.

39. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbali mbali kwa ajili ya kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo:-

i. Kuendelea kuweka bei elekezi na kusimamia bidhaa mbali mbali zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;

ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya shilingi ya Tanzania na kudhibiti mfumuko wa bei utakaochochea ukuaji wa uchumi;

iii. Kuimarisha programu za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa chakula;

iv. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali, itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine;

v. Kushajiisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;

vi. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula na kudhibiti bei nchini; na

vii. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024

40. **Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 umejikita katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa mwaka 2021-2026 (ZADEP), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025 na Maelekezo, Hotuba na Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mpango huu utatekeleza miradi na programu ambazo utekelezaji wake una azma ya kufikia malengo yaliyowekwa na Dira ya Maendeleo ya mwaka 2050. Hivyo, miradi ya kimkakati kwa mwaka 2023/2024 inalenga kufanikisha malengo yaliyoanishwa katika maeneo matano (5) ya Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa Miaka Mitano 2021–2026. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

## Maeneo ya Kimkakati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

41. **Mheshimiwa Spika**, Maeneo ya kimkakati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni: (1) Kutumia fursa za Uchumi wa Buluu; (2) Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu; (3) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; (4) Kukuza Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; na (5) Kuimarisha Utawala na Uhimili.

### I. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

42. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na juhudi zake za kuongeza fursa za bahari kuchangia Pato la Taifa na upatikanaji wa ajira. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi Mangapwani pamoja na ujenzi wa Diko na Soko la Kisasa la Samaki unaotarajiwa kufanyika katika eneo la Kama. Takriban TZS 23.5 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kutekelza shughuli hizo.

### II. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

43. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatambua kuwa miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikabili nchi yetu kwa sasa ni suala la usafirishaji wa mizigo, kutokana na kuwa na miundombinu hafifu ya Bandari. Hivyo, Serikali inaendea na shughuli za utafutaji wa mwekezaji wa ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani (Intergrated Port) kulingana na Mpango Mkuu (Master Plan) itakayojumuisha bandari za Mizigo, Chelezo, Mafuta na Gesi, kuendelea kwa matengenezo ya bandari ya Mkoani pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa Bandari ya Wete kwa lengo la kuijenga upya.

44. **Mheshimiwa Spika**, hatua za matayarisho ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba zimekamilika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali inatarajia kukamilisha uhakiki na kuanza shughuli ya ulipaji wa fidia ambapo jumla ya TZS

10 bilioni zitatumika kuwalipa fidia wananchi watakaoathirika wakati wa ujenzi wa kiwanja hicho. Jumla ya TZS 150 bilioni zinatarajiwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo kama ni mkopo kwa ajili ya ujenzi. Aidha, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi.

45. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na uimarishaji wa miundombinu ya barabara mbalimbali Unguja na Pemba, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa barabara mbali mbali Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 782.9 ikiwemo barabara ya Mkoani – Chake Chake km 43.5, Fumba – Kisauni km 12, Tunguu – Makunduchi km 48, Chake Chake – Wete km 22.1, Barabara Kuu zenye urefu wa kilomita 277, Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 pamoja na Barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa Kilomita 100.9. TZS 373.5 bilioni zinatarajiwa kutumika katika ujenzi wa barabara hizo.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha huduma ya usambazaji maji safi na salama nchini, Serikali imepanga kutumia TZS 77.5 bilioni kuendelea na Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji wa Maji Safi na Salama pamoja na usimamizi wa rasilimali za vyanzo vya maji. Sambamba na hayo, sekta ya nishati itaimarishwa kwa upatikanaji wa nishati mbadala ya umeme kutokana na nguvu za jua kupitia mradi wa Mageuzi wa Sekta ya Nishati ZESTA (Zanzibar Energy Sector Transformation and Accessibility-ZESTA). Serikali inatarajia kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika wakati wa ujenzi wa njia za kusafirishia umeme na maeneo ya uzalishaji umeme. Jumla ya TZS 7.2 bilioni zimetengwa na Serikali kwa ajili ya ulipaji wa fidia, fedha za utekelezaji wa mradi TZS 8.9 bilioni zinatarajiwa kutoka Benki ya Dunia.

## III. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

47. **Mheshimiwa Spika**, Uchumi wa Zanzibar unaendeshwa na sekta chache zenye kuzalisha ajira na kutoa mapato. Mkazo unawekwa katika kutumia njia mbalimbali za kiuchumi kupitia uchumi wa buluu kwa kuendeleza uwekezaji wa ndani, uwazi wa biashara, maendeleo ya rasilimali watu, viwanda vidogo, uimarishaji wa zao la karafuu, mwani na mazao ya viungo, utalii na usafirishaji.

## IV. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

48. **Mheshimiwa Spika**, Maendeleo ya jamii yanajumuisha taaluma, ujuzi na afya ambayo watu wamewekeza katika maisha yao na kuwezesha kuwa miongoni mwa wazalishaji katika jamii. Serikali itaendelea kuimarisha rasilimali watu sambamba na huduma za jamii ili ziweze kuleta tija na manufaa katika jamii. Katika kufanikisha hilo, Serikali inakusudia kuimarisha sekta ya Afya kwa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Ujenzi na uimarishaji wa nyumba za madaktari; Ujenzi wa hospitali ya Binguni ambayo itakua ni Taasisi ya Tiba, tafiti na kufundishia, jumla ya TZS 30.0 bilioni zinatarajiwa kutumika. Aidha, kwa upande wa sekta ya elimu Serikali inatarajiwa kuendelea na Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu (kujenga na kuimarisha miundombinu ya skuli, dakhalia na madarasa, maktaba, samani, maabara, nyumba za walimu na kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kujifunza na kufundishia, kuandaa walimu na mitaala mipya) ambapo TZS 64.0 bilioni.

49. **Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali inatarajia kutekeleza Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (Boosting Inclusive Growth for Zanzibar- Big-Z); ambayo itahusisha uimarishaji wa mitaa mbalimbali kwa ujenzi wa miundombinu ya uimarisjhaji mitaa hiyo ikiwemo ujenzi wa

barabara na ujenzi wa mitaro ya maji taka. Vile vile, Serikali imepanga kufanya matengenezo makubwa katika kiwanja cha mpira Amani na kuanza ujenzi wa Viwanja vya michezo vya wilaya,  TZS 33 bilioni zimepangwa kutumika.

### V. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili

50. **Mheshimiwa Spika,** Utawala bora na uhimili ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika Taifa lolote. Mpango huu umezingatia utawala bora wa kiutendaji ili kukabili vihatarishi vya madhara, ujumuishaji kwa kufanya tathmini kwa vitendo kwa kufuata miongozo na taratibu zilizopo.

51. **Mheshimiwa Spika**, Ulinzi na usalama ni sehemu muhimu ya kuimarisha utawala bora hivyo Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Ulinzi na Usalama. Katika kukuza ufanisi wa utoaji wa huduma za umma juhudi za kuhakikisha mazingira mazuri kwa wafanyakazi Serikali inaendelea na utanuzi na ukarabati wa Ofisi mbali mbali za Umma pamoja na kuanza ujenzi wa Mji mpya wa Serikali katika eneo la Kisakasaka. Jumla ya  TZS 94.1 bilioni zimepangwa kutumika kwa mwaka 2023/2024.

52. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali inatarajia kutekeleza Miradi mengineyo ambayo itagharimu TZS 434.4 bilioni. Sehemu kubwa ya Miradi mengineyo ni Miradi inayoendelea, malipo ya fidia na upelekaji wa miundombinu katika maeneo yanayotarajiwa kutekelezwa miradi ya kimkakati kama inavyoonekana katika Kitabu cha Pili.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024

53. **Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 umepangwa kutumia jumla ya TZS 1,521.99 bilioni

(ikijumuisha TZS 1,514.79 bilioni za miradi halisi ya maendeleo ya Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni za maendeleo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa) Aidha, miradi mingine ya maendeleo, itaendelea kugharamiwa na sekta binafsi na utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

## MAENEO MTAMBUKA

### Matumizi ya Matokea ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022

54. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mara nyengine, Tanzania ikiwemo Zanzibar imekamilisha ripoti ya sensa ya idadi ya watu na makaazi ya mwaka 2022. Takwimu hizi za msingi ndizo zinazowezesha kuainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi maalum yenye uhitaji maalum kwa mfano, watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo. Kufuatia kukamilika zoezi hilo ripoti tayari zimetolewa na takwimu za ripoti hizo zimezingatiwa katika kuandaa Mipango ya Serikali.

55. **Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Sensa hiyo yalitangazwa rasmi mwezi Oktoba mwaka 2022 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo kwa upande wa Zanzibar, idadi ya watu imefikia 1,889,773 kati ya hao wanaume ni 915,492 sawa na asilimia 48.4 na wanawake ni 974,281 sawa na asilimia 51.6. Idadi hii ya watu wa Zanzibar inakua kwa asilimia 3.7 kwa mwaka, ukuaji ambao si rafiki ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wetu. Pia kwa mujibu wa Sensa ukuaji huu wa idadi ya watu unachangiwa zaidi na kuzaliana ambapo inaonekana kiwango cha jumla cha uzazi (Total Fertility Rate) ni 4.7. Mkoa wa Mjini Magharibi ndio

unaoongoza kwa idadi kubwa ya watu wanaofikia 893,169 sawa na asilimia 47.2 ya watu wote wa Zanzibar.

## Uhifadhi wa Mazingira

56. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha uhifadhi wa mazingira kwa misingi ya kisheria unaimarika, Serikali imepanga kufanya mapitio ya Sera ya Mazingira ya mwaka 2013, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015 ili kuendana na hali ya sasa. Utayarishaji wa Mpango wa Kitaifa wa Mazingira pamoja na tafiti ya kuyatambua maeneo yaliyoathirika kimazingira yaliyotokana na mabadiliko ya tabianchi na kuyahuisha maeneo hayo. Vile vile, kujenga uwezo wa wakulima wadogo kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakuwa na matokeo yenye tija sambamba na kushajihisha uhifadhi wa Mazingira kwa upandaji miti katika Wilaya zote ili kuimarisha na kuhuisha uoto wa asili pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji na rasilimali zisizorejesheka. Vile vile tathmini ya kina itaendelea kufanyika ili kupata taarifa sahihi na kuweka mkakati madhubuti wa usimamizi endelevu wa ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa wavuvi wadogo katika Eneo la Hifadhi ya Mkondo wa Pemba. Zanzibar pia, imeandaa Programu ya Urithi wa Kijani, ambapo kila mwananchi atastahiki kushiriki katika utekelezaji wake.

## Makundi yenye Mahitaji Maalum (Ulemavu, Dawa za Kulevya na UKIMWI)

57. **Mheshimiwa Spika**, Ili kuhakikisha tunakuza haki na fursa kwa Watu wenye ulemavu, jumla ya visaidizi 852 Unguja na Pemba, kwa upande wa Unguja 469 (wanawake 240 na wanaume 229) na kwa Pemba visaidizi 383 (wanawake 250 na wanaume 133). Usajili na uhakiki wa taarifa za Watu wenye Ulemavu unaendelea ili kupata taarifa sahihi zitakazosaidia katika kuandaa mipango mbali mbali ya Baraza. Ujumuishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu katika programu mbali mbali za kitaifa na kimataifa limepewa kipaumbele na kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanafikia huduma kwa urahisi. Katika kipindi hiki, kupitia Baraza Serikali imetenga fedha za ruzuku

kwa ajili ya kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa maendeleo ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar.

58. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza imeanzisha Kituo Jumuishi (Transnational Organized Crime Unit) kwa ajili ya kuongeza kasi ya ushughulikiaji wa kesi zinazohusu uhalifu wa kupangwa ikiwemo dawa za kulevya. Kituo hicho kimeanza kazi na kinashirikisha watendaji kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, jitihada za kurekebisha tabia na hali za watumiaji wa dawa za kulevya zitaendelea kupitia nyumba za upataji nafuu na kituo cha Serikali kilichopo Kidimni, ambacho pia kimeweka utaratibu wa kuwaunganisha na kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali baada ya kupata matibabu. Aidha, jumla ya waathirika 186 wa madawa wamepokelewa kati ya hao 40 wameruhusiwa baada ya kukamilisha huduma ya tiba 35 wameondolewa kwa sababu mbali mbali, 60 wametoroka, 51 wanaendelea kupata huduma na 15 wamerekebishika tabia na kuacha kutumia madawa ya kulevya watu hao kwa sasa wanaendelea kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali ikiwemo ufugaji wa kuku, ng’ombe na ushoni.

59. **Mheshimiwa Spika**, Kwa lengo la kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya UKIMWI, Serikali imo katika hatua za kuingiza kipengele cha masuala ya UKIMWI katika Muongozo wa Uandaaji wa Miradi ya Maendeleo ili kuhakikisha kwamba maambukizo ya VVU yanadhibitiwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo husika. Pia, Muongozo wa Kuandaa Mipango ya Kudhibiti maambukizo ya VVU na UKIMWI katika miradi mikubwa ya maendeleo ambao utatumiwa na sekta mbali mbali umeandaliwa. Vile vile, Mkakati wa Mawasiliano na Mabadiliko ya tabia kwa vijana utaandaliwa pamoja na kuifanyia mapitio Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI ili iweze kwenda sambamba na hali ya sasa na mabadiliko ya kisayansi ya kinga na tiba ya VVU na UKIMWI.

## Tafiti na Ubunifu

60. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha mipango yetu inakwenda sambamba na mahitaji ya nchi, Serikali imedhamiria kuimarisha upatikanaji wa matokeo ya tafiti na ubunifu ili kuweza kuongeza ushahidi wa kisayansi katika kufanya maamuzi, kuimarisha sera na kutoa majibu ya kisayansi. Kwa sasa, Serikali imeweza kuimarisha mfumo wenye taarifa za tafiti na ubunifu, kuwapatia mafunzo watafiti, na kufanya tafiti za kimkakati za vipaumbele vya tafiti katika maeneo ya kiuchumi na kijamii. Tunaziomba Wizara/Idara na Taasisi za Serikali kulipokea na kulipa msisitizo suala la tafiti na ubunifu ili kuweza kuipatia Serikali matokeo sahihi ya kuweza kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza nchini.

## Mipango ya Kuendeleza Watenda Kazi

61. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha Zanzibar inafikia dhamira ya Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 ya Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji wa Maendeleo Jumuishi na Endelevu, Serikali imekamilisha mapitio ya vipaumbele vya elimu vya Taifa. Aidha, Serikali inaendelea kuwaandaa watenda kazi wa baadae kufanya maamuzi sahihi wakiwa katika ngazi za elimu ya sekondari ili waweze kuzitambua kada adimu na fani za vipaumbele kwa mujibu wa mahitaji ya soko la ajira linalotokana na Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Sambamba na hayo, Mpango wa Kuimarisha Ujuzi na Taaluma kwa Wafanyakazi unaandaliwa ili kuwawezesha wafanyakazi kupata fursa za kujiendeleza kitaaluma kwa mujibu wa kada na majukumu yao ya kazi. Vile vile, kanzidata ya kufuatilia wahitimu wa elimu za juu yenye lengo la kuwatambua na kujua mahitaji halisi ya soko la ajira kwa kila fani na kada walizosomea pamoja na kuziunganisha Taasisi zinazohusika katika kuzalisha wataalamu zikiwemo Vyuo Vikuu, Bodi ya Mikopo na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

## UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI

62. **Mheshimiwa Spika**, Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa ni moja ya nyenzo muhimu inayopima ufanisi wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo. Serikali itaendelea kutumia mbinu na viashiria vilivyoainishwa katika Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2021–2026 ili kupima utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 na kuchukua hatua zitakazohakikisha malengo ya utekelezaji yanafikiwa. Miongozo mbali mbali ya ufuatiliaji na tathmini ya Mpango ikiwemo Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 itaendelea kuzingatiwa. Tume ya Mipango inaendelea kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E System) kwa ajili ya kuimarisha uratibu wa ufuatiliaji na tathmini ili kupata matokeo tarajiwa.

63. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Serikali imefanikiwa kutekeleza Malengo yote Kumi na Saba (17) ya Maendeleo Endelevu hususan katika Malengo matano (5) ya kimkakati yaliyowekwa kwa Dunia nzima katika kuhakikisha nchi zote zinastawi kimaendeleo kutokana na Athari za maradhi ya mripuko ya Uviko-19. Malengo hayo yanajumuisha: Lengo nambari 6, Kuhakikisha Upatikanaji wa Maji Safi na Salama; Lengo nambari 7, Kuhakikisha Upatikanaji wa Nishati Mbadala kwa Gharama Nafuu; Lengo nambari 9, Kukuza Viwanda, Ubunifu na Miundo mbinu; Lengo nambari 11 Kufanya Miji kuwa Jumuishi, Salama na Jamii Endelevu; na Lengo namba 17, Kukuza Ushirikiano wa Kimataifa kwa Maendeleo Endelevu. Mafanikio katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaonekana katika Programu na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali yetu ambayo imeanza kuleta tija kwa wananchi na wakaazi wote wa Zanzibar.

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo, Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Maendeleo wa Zanziabar umeandaliwa kwa ajili ya kuongoza wadau wote wa maendeleo kutekeleza maeneo ya kimkakati na kipaumbele kwa kupima Utekelezaji wa Mpango wa Maendelo. Muongozo huu ni wa miaka mitano 2021–2026 ambao una lengo la kupima matokeo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya kufikia Malengo na Mikakati iliyoundwa.

65. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia umuhimu wa taarifa za utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo, Serikali imeandaa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kutoa muongozo na kusimamia maswala yote ya Ufuatiliaji na Tathmini nchini. Sera hiyo ipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuanza kutumika. Aidha, mafunzo ya uelewa wa Sera hiyo yatatolewa kwa Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sekta binafsi ili kila Sekta ifahamu na kuweza kuitumia kwa maendeleo ya dhana ya Ufuatiliaji na Tathmini nchini kwa ajili ya kuleta uwajibikaji katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo.

66. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza matayarisho ya kufanya mapitio ya Mpango wa kati wa Maendeleo (ZADEP) 2021-2026 kwa kipindi cha utekelezaji wake kwa miaka miwili ili kujua mafanikio na changamoto, kufanya uchambuzi na kuja na mapendekezo ya kuishauri Serikali kwa ajili ya Maendeleo ya Zanzibar. Vile vile, inaendelea kuandaa Rasimu ya Ripoti ya Hiari ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (VNR 2023) na kuiwasilisha katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuunganishwa na ya Tanzania Bara na kupata ripoti moja ya Kitaifa kwa kuwasilishwa Umoja wa Mataifa.

67. **Mheshimiwa Spika,** Tathmini imefanyika kwa baadhi ya Miradi ikiwemo Mradi wa Zanzibar Salama na Programu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar ili kuleta matokeo chanya kama ilivyokusudiwa katika miradi hiyo. Kutokana na umuhimu wa miradi kitaifa, Serikali itaendelea kufanya Tathmini katika Miradi mengine mara kwa mara ili kuweza kuleta uwajibikaji katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka. Kwa kuhakikisha Mradi wa Zanzibar Salama na Programu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar inakuwa na tija zaidi kwa nchi, Serikali iliziagiza Wizara husika kufanyia kazi baadhi ya maeneo yatakayoimarisha uendelevu na maslahi makubwa kwa wananchi.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande Mradi wa Zanzibar Salama, Wizara husika iliagizwa kufanya matengenezo ya miundombinu za mradi, kuhakikisha vifaa vyote vya mradi vinatumika kama vilivyopangwa na kuhakikisha wanapata mafunzo ya mfumo wa uendeshaji wa kamera (Command and Control System) na kuweza kuusimamia bila ya Mtaalamu kutoka nje. Kwa Programu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar, Wizara husika iliagizwa kufanya Utafiti wa mazao mbadala yatakayoleta tija kwa nchi, kutathmini utekelezaji wa kilimo cha mpunga kwa kupata uzoefu kutoka kwa wakulima na wawekezaji wa mashamba ya Mbarali na kuliendeleza eneo lililobakia la hekta 7,468 zinazoweza kulimwa kwa umwagiliaji baada ya kuhakikisha halimilikiwi na wananchi.

## MAJUMUISHO

69. **Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024 ni njia ya kuelekea uchumi wa kati katika kipato cha juu unaolenga kuimarisha maisha bora, amani, utulivu, utawala bora, jamii iliyoelimika, afya bora na kuwa na uchumi shirikishi na shindani. Kwa kutambua mchango na umuhimu wa sekta binafsi, Mpango huu umeipa sekta binafsi umuhimu

mkubwa. Vile vile, Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza miradi shirikishi (PPP) katika kugharamia utekelezaji wa mpango.

70. **Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie kwa kusisitiza kuwa utekelezaji wa Mpango huu unatuhusu kila mmoja wetu, hivyo nasisitiza kuwa mashirikiano yetu sote katika ngazi mbali mbali ili kufikiwa malengo yetu ya kukuza uchumi wa Zanzibar. Naomba pia, nitoe wito kwa kila sekta kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ipasavyo katika eneo lake la kiutendaji.

**HITIMISHO**

71. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati na kwa niaba ya Serikali ninaomba kutumia fursa hii adhimu ya kuwashukuru wadau wote wa maendeleo wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Washirika wa Maendeleo na Wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika mipango, utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na kujenga uchumi wa nchi yetu. Ushiriki wao wa dhati umewezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ninawaomba waendelee kutupa ushirikiano katika kutekeleza Mpango huu ili kufikia malengo tuliyojiwekea.

72. **Mheshimiwa Spika,** Naomba niwatambue Washirika wa Maendeleo wa ndani kwa Mwaka 2023/2024 kama ifuatavyo: PBZ, ZSSF, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, NMB, NBC, CRDB na COSTECH. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo wa nje na nchi rafiki zinazoendelea kushirikiana nasi kwa mwaka 2023/2024 ni pamoja na ACRA, AF, AFD-FRANCE, AfDB, AMREF, AUSTRIA, BADEA, BELGIUM, CHINA, CANADA (CIDA), DANIDA, DfID, EDF, EU, EXIM BANKS za India, China na

Korea, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, GERMANY (GIZ AND KfW), GPE, GOOD NEIGHBOURHOOD, HIPZ, IAEA, INDIA, IFAD, ILO, IMF, IRELAND, JAPAN (JICA), KHALIFA FUND, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOREA, KUWAIT, MALAYSIA, NORWAY, OMAN, OPEC FUND, PMI, QATAR CHARITY ORGANISATION, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, STBF, SWEDEN, THPS, TfT, UK, UKEF/CITI BANK NA DEUTCH BANK, UN, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UNIDO, USAID, UN WOMEN, UTURUKI, WORLD BANK na WHO. Kipekee naomba nitoe shukrani kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana Zanzibar katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

73. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nitoe shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Mheshimiwa Ali Suleiman Mrembo ambaye ni msaidizi wangu wa karibu kwa umakini wake, busara na weledi katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu. Pia, nawashukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ushirikiano wao katika maandalizi ya hotuba hii. Aidha, ninawashukuru Makamishna wa Tume ya Mipango Nd. Mohammed Masoud Salim, Kamishna wa Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini, Dkt Zuhura Mohamed Abdallah, Kamishna wa Ufuatiliaji na Tathmini, Dkt Afua Khalfan Mohamed Kamishna wa Utafiti, Dkt. Ameir Haji Sheha, Kamishna wa Ukuzaji Uchumi; Dkt Rukkaya Wakif Muhammed, Kamishna wa Maendeleo ya Watendakazi; na watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salim Mahfoudh. Vile vile niwashukuru Katibu Mkuu Ofisi ya Rais -Fedha na Mipango Dkt Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu Nd. Aboud Hassan Mwinyi na Mhasibu Mkuu wa Serikali Dkt. Said Seif

Mzee kwa kufanyakazi kwa karibu na Tume ya Mipango.

74. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kumaliza hotuba yangu hii, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wawakilishi na Wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inaambatanishwa na vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2022 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/2023 na Mwelekeo wa Hali ya uchumi wa Zanzibar 2023 na Mpango wa Maendeleo wa 2023/2024 ambavyo vina taarifa na uchambuzi wa kina vinapatikana katika tovuti ya Tume ya Mipango (http.planningznz.go.tz)

75. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Baraza lako Tukufu lipokee na kujadili Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/2024.

76. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima naomba kutoa hoja.

**DKT. SAADA MKUYA SALUM**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**
**ZANZIBAR**